# UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE

## VYA BAJETI VYA MWAKA 2022/23 NA VIPAUMBELE VYA MWAKA 2023/24

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Nishati





DODOMA
MEI, 2023

# 1.0 UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA MWAKA 2022/2023

## 1

Kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme, ikiwemo kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa kwenye mikoa ya Katavi, Kigoma na Kagera na mradi mkubwa wa Kuimarisha Gridi ya Taifa *(National Grid Stabilization Project).*

### A. Uzalishaji wa Umeme:

1. Uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa umeongezeka kwa asilimia 10.5 na kufikia MW 1,872.05 ikilinganishwa na MW 1,694.55 za mwaka 2021/22.
2. Utekelezaji wa Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) – MW 2,115, umefikia asilimia 86.89 ikilinganishwa na asilimia 60.22 za mwezi Aprili, 2022
3. Hadi kufikia tarehe 23 Mei, 2023 kina cha maji ya Bwawa la JNHPP kilifikia mita 160.51 kutoka usawa wa bahari ambapo ili kuweza kuzalisha umeme, kiwango cha chini cha maji kinatakiwa kufikia mita 163 kutoka usawa wa bahari. Aidha, hadi kufikia tarehe hiyo, kiwango cha maji kilifikia mita za ujazo bilioni 11.8 sawa na asilimia 39.3 ya kiwango cha juu ambacho ni mita za ujazo bilioni 30.
4. Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185 umekamilika na kuchangia MW 185 katika Gridi ya Taifa. Utekelezaji wa mradi huo mwaka 2021/22 ulikuwa asilimia 88.
5. Utekelezaji wa Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rusumo – MW 80 umefikia asilimia 99 ikilinganishwa na asilimia 91.6 za mwaka 2021/22.
6. Taratibu za upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme ya Kakono (MW 87) na Malagarasi (MW 49.5) zimekamilika.
7. Miradi mingine ya kuzalisha umeme, ikiwemo kwa kutumia maji ya Ruhudji – MW 358, Kikonge – MW 321 na Rumakali – MW 222 na kwa kutumia Jua mkoani Shinyanga – MW 150 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.



## B. Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme

1. Miundombinu ya kusafirisha umeme imeongezeka na kufikia jumla ya urefu wa kilomita 6,363.27 sawa na ongezeko la asilimia 4.1 ikinganishwa na kilomita 6,111.27 zilizokuwepo hadi kufikia mwezi Mei, 2022;
2. Miundombinu ya kusambaza umeme imeongezeka na kufikia kilomita 168,548.36 sawa na ongezeko la asilimia 9.5 ikilinganishwa na kilomita 153,988.49 zilizokuwepo hadi kufikia mwezi Mei, 2022;
3. Mradi wa Kusafirisha Umeme kutoka JNHPP hadi Chalinze – kV 400 umefikia asilimia 93.5 ikilinganishwa na asilimia 44 mwaka 2021/22. Aidha, ujenzi wa kituo cha Kupoza Umeme cha Chalinze ambacho ni sehemu ya mradi huo umefikia asilimia 64 ikilinganishwa na asilimia 3.59 mwaka 2021/22.
4. Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi umekamilika. Utekelezaji wa mradi huo ulikuwa asilimia 99 mwaka 2021/22.
5. Utekelezaji wa mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga umefikia asilimia 95 ikilinganishwa na asilimia 79.3 mwaka 2021/22.
6. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi umekamilika, ambapo utekelezaji wake ulikuwa asilimia 79 mwaka 2021/22.
7. Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa *(National Grid Stabilization Project)* umeendelea kutekelezwa kwa kuunganisha Mkoa wa Kigoma katika Gridi ya Taifa kupitia kituo cha Nyakanazi na kuunganisha Wilaya za Ngara na Biharamulo kwenye kituo cha Gridi ya Taifa Nyakanazi.
8. Serikali kupitia TANESCO inatekeleza jumla ya miradi 48 ikijumuisha miradi 20 ya kuongeza uwezo wa miundombinu ya usafirishaji umeme, miradi 12 ya kuboresha mifumo ya uendeshaji wa Gridi ya Taifa na miradi 16 ya ukarabati wa miundombinu ya usafirishaji umeme.
9. Ilisainiwa mikataba 26 baina ya Serikali na Wakandarasi yenye thamani ya shilingi trilioni 1.9 ya kutekeleza miradi mbalimbali ya kuimarisha Gridi ya Taifa.
10. Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Katavi umefikia asilimia 26.7.



11. Serikali imetoa Shilingi bilioni 16.43 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi 6,500 wanaopisha mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma (TAZA) na Wananchi 4,750 tayari wamelipwa fidia zao.
12. Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Morogoro hadi Dodoma kwa ajili ya uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot II) umefikia asilimia 98 ikilinganishwa na asilimia 88 mwaka 2021/22.
13. Jumla ya wateja 4,319,258 wameunganishiwa umeme hadi mwezi Aprili, 2023, ikiwa ni ongezeko la asilimia 12.4 ikilinganishwa na wateja 3,842,096 waliokuwepo mwezi Juni, 2022.
14. Miradi mbalimbali ya usafirishaji umeme, ikiwa ni pamoja na Msongo wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma na Tabora hadi Kigoma kupitia Urambo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

# 2

## Kutekeleza Miradi ya Nishati Vijijini pamoja na kuanza utaratibu wa kupeleka umeme katika Vitongoji vyote nchini.

1. Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (REA III Round 2) umefikia asilimia 68.66 ambapo vijiji 1,880 kati ya 4,071 sawa na asilimia 46.18 vimeunganishiwa umeme na vijiji vyote Tanzania Bara vitakuwa vimeunganishiwa umeme ifikapo mwezi Juni, 2024. Hadi sasa jumla ya vijiji 10,127 vimeungiwa umeme sawa na asilimia 82 ya vijiji vyote.
2. Utekelezaji wa mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji – *(Hamlet Electrification Project – HEP)* umeanza ambapo zoezi la kuwapata wakandarasi kwa ajili ya kupeleka umeme katika vitongoji 654 vilivyopo katika Mikoa ya Songwe na Kigoma lipo katika hatua za mwisho.
3. Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili B unaolenga kuongeza wigo wa usambazaji umeme kwenye vitongoji 1,686 katika mikoa ya Arusha, Geita, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Morogoro, Njombe na Songwe na kuunganisha jumla ya wateja wa awali 95,334 uliendelea kutekelezwa kwa Wakandarasi kufanya upimaji wa njia za ujenzi wa mradi, kuandaa michoro pamoja na ununuzi wa vifaa.
4. Taratibu za kuwapata Wakandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili C zilikamilishwa. Mradi huo unalenga kuongeza wigo wa usambazaji umeme kwenye vitongoji 1,880 katika mikoa ya Manyara, Iringa, Rukwa, Mtwara, Ruvuma, Simiyu na Mara kwa kujenga kilomita 6,562 za msongo mdogo na kufunga mashineumba 1,932 ili kuunganisha wateja wa awali 131,719.
5. Utekelezaji wa Mradi wa Peri Urban Awamu ya Pili ulifikia asilimia 91.0 ikilinganishwa na asilimia 84.4 mwaka 2021/22. Mradi huu unahusisha kupeleka umeme katika maeneo 153 yaliyopo katika majiji ya Arusha, Dodoma na Mwanza kwa kujenga miundombinu ya kusambaza umeme yenye urefu wa kilomita 751, kufunga mashineumba 143 na kuunganisha wateja wa awali 16,328.
6. Jumla ya mikataba nane (8) ilisainiwa na Wakandarasi watano (5) kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi wa Peri Urban Awamu ya Tatu katika mikoa nane (8) ya Geita, Kigoma, Kagera, Mbeya, Mtwara, Singida Tabora na Tanga na wakandarasi hao wamekamilisha upimaji na usanifu na wanaendelea na kazi ya ununuzi wa vifaa na kuanza ujenzi wa miundombinu.
7. Serikali imepata waendelezaji sita (6) wa miradi ya kusambaza umeme kwa kutumia nguvu ya jua, itakayotekelezwa katika visiwa 36. Wakandarasi hao wanaendelea na Upembuzi Yakinifu, kuandaa Mpango wa Biashara, Vyeti vya Athari za Mazingira na Hati ya Kinga ya Malipo ya Awali *(Advance Payment Gurantee)*.

8. Umeandaliwa Mwongozo na Kanuni za Utoaji Mikopo kwa waendelezaji wa ujenzi wa vituo vidogo vya mafuta vijijini. Aidha, fursa za mikopo husika zimetangazwa na waombaji wanatakiwa kuwasilisha maombi hadi kufikia tarehe 30 Agosti, 2023.

9. Wamepatikana Wakandarasi wanne (4) kwa ajili ya kusambaza umeme katika Vituo vya Afya 66 na Pampu za Maji 333 vilivyopo vijijini katika mikoa 25 Tanzania Bara. Wakandarasi hao wamekamilisha usanifu wa mradi na kuendelea na ununuzi wa vifaa pamoja na kuanza ujenzi wa miundombinu ya mradi.

10. Jumla ya taasisi 43,925 zinazotoa huduma kwa jamii ikiwemo za Elimu, Biashara, Pampu za Maji, Vituo vya Afya na Nyumba za Ibada zimeunganishiwa umeme ikilinganishwa na taasisi 40,408 mwaka 2021/22.

11. Wamepatikana wakandarasi kwa ajili ya kupeleka umeme katika maeneo 336 ya wachimbaji wadogo wa madini, maeneo ya kilimo na viwanda katika maeneo mbalimbali Tanzania Bara. Wakandarasi hao wanaendelea na zoezi la upimaji wa kina wa njia za kusambaza umeme na ununuzi wa vifaa.

12. Serikali imefanya utambuzi wa wigo wa mradi wa Kupeleka Umeme katika Shule na Mahakama za Mwanzo Vijijini ambapo jumla ya shule 729 na mahakama 292 zimebainishwa kuwa na uhitaji wa kuunganishiwa umeme. Aidha, REA na TANESCO wapo katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za kuanza utekelezaji wa mradi huu.

13. Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuimarisha utekelezaji wa miradi ya nishati vijijini ikiwa ni pamoja na kuajiri Waratibu wa miradi ya nishati vijijini kwa Wilaya zote za Tanzania Bara; kutoa kibali cha kuajiri Wahandisi 20 wa miradi ya REA na kununua magari 21 yatakayotumika katika usimamizi wa miradi ya REA katika mikoa mbalimbali nchini.



## 3

### Kukamilisha mazungumzo ya mradi wa LNG Lindi na kuanza maandalizi ya utekelezaji wake.

1. Mazungumzo ya mradi wa LNG yamekamilika kwa kuandaliwa kwa Mikataba miwili mikubwa ambayo ni Mkataba wa Nchi Hodhi na Mkataba wa Uzalishaji na Ugawanywaji Mapato (PSA).
2. Serikali tayari imeanzisha Ofisi ya Mradi wa LNG kwa ajili ya kuratibu, kuwezesha na kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya mradi kwa tija na ufanisi ili manufaa yake yapatikane kwa wakati kama ilivyokusudiwa.



## 4

### Kutekeleza miradi ya nishati jadidifu ikiwemo jotoardhi, tungamotaka, upepo na jua pamoja na matumizi bora ya Nishati (*Energy Efficiency and Conservation*).

1. Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kupitia jotoardhi ya Ngozi (Mbeya) - MW 70, Songwe (Songwe) - MW 5, Kiejo-Mbaka (Mbeya) – MW 60, Natron (Arusha) – MW 60 na Luhoi (Pwani) – MW5.
2. Umenunuliwa mtambo wa kuchoronga visima vya uhakiki (*drilling rig*) kwa miradi ya jotoardhi. Kupatikana kwa Mtambo huu kutawezesha uchimbaji kwa maeneo yote yaliyoainishwa kuwa na viashiria vya jotoardhi na kupata matokeo stahiki kwa haraka.
3. Bei elekezi za Kampuni sita (6) za wazalishaji wadogo wa umeme ziliidhinishwa. Bei hizi zinaendelea kuhamasisha na kuchochea uwekezaji binafsi katika uzalishaji umeme.
4. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, kulikuwa na jumla ya Wazalishaji Wadogo 17 waliozalisha jumla ya MW 70.17 kupitia vyanzo mbalimbali vya nishati jadidifu, ikiwa ni pamoja na tungamotaka, jua na mvuke.
5. Maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa Nishati ya Tungamotaka yalianza kwa kukamilisha Hadidu za Rejea kwa ajili ya Mshauri Mwelekezi wa kuandaa Mkakati huo pamoja na kukusanya maoni ya wadau kuhusu masuala muhimu ya kuzingatiwa katika Mkakati huo.
6. Serikali ilianza kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Nishati na uhuishaji wa Mpango wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Nishati ili kuendana na mahitaji halisi ya matumizi bora ya nishati kwa sasa.

# 5

## Kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha nchini, ikiwemo uanzishwaji wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta (*Strategic Petroleum Reserve*) na Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya Bei za Mafuta (*Fuel Price Stabilization Fund - FPSF)*.

1. Nchi imeendelea kuwa na uhakika wa usalama wa upatikanaji wa mafuta kwa kuhakikisha uwepo wa akiba ya mafuta ya kutosha.

2. Yaliwasilishwa Serikalini mapendekezo ya kuanzisha Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya Bei za Mafuta (*Fuel Price Stabilization Fund*). Kwa sasa tathmini inaendelea kufanyika kuhusu vyanzo vya fedha za mfuko huo ili uwe endelevu kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa, pamoja na muda muafaka wa kuanzisha kwa kuzingatia mwenendo wa bei za mafuta katika soko la Dunia.

# 6

## Kuiimarisha TPDC na Kampuni zake Tanzu za TANOIL na GASCO.

1. Serikali iliridhia kubadili mkopo wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba na Mitambo ya Kuchakata Gesi Asilia wa Dola za Marekani 1,193,611,687.49 kuwa mtaji wa Serikali kwa TPDC. Hatua hii itaimarisha Mizania ya Hesabu (Balance Sheet) za TPDC na hivyo kuliwezesha Shirika hilo kuvutia uwekezaji katika utafutaji na uendelezaji wa shughuli za mafuta na gesi na kuimarisha mapato.

2. Utendaji wa TPDC umeendelea kuimarishwa, ikiwa ni pamoja na kuunda Bodi ya Shirika hilo inayoongozwa na Balozi Ombeni Sefue (Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu), na kufanya mabadiliko makubwa kwenye menejimenti ya shirika hilo. Aidha, Serikali imeondoa menejimenti yote ya Kampuni tanzu ya TANOIL na kutengeneza mkakati mpya wa biashara na uendeshaji wa kampuni hiyo.



# 7

## Kuboresha miundombinu ya kupokea, kushusha, kuhifadhi na kutoa mafuta katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na Ghala za dhamana ya forodha *(Customs Bonded Warehouse)* na Kituo cha Pamoja cha kupokelea Mafuta kutoka Melini *(Single Receiving Terminal)*.

1. Serikali kupitia Wizara ya Nishati ilisaini Mkataba wa Makubaliano (MoU) na Kampuni ya ENOC LLC ya Falme za Kiarabu kwa ajili ya ujenzi wa kituo kikubwa cha kupokea na kuhifadhi mafuta jijini Dar es Salaam. Aidha, tayari eneo la kujenga kituo hicho limepatikana na Serikali ilishaunda Kikosi Kazi kinachosimamia utekelezaji wa mkataba ulioingiwa.

2. Kampuni ya TIPER iliendelea na ujenzi wa matenki mawili yenye ukubwa wa lita milioni 30 kila moja ili kuongeza uwezo wa kupokea na kuhifadhi mafuta kama Kituo cha Kupokea Mafuta kwa Pamoja *(Single Receiveing Terminal - SRT)*. Aidha, TIPER iliendelea kusimika pampu za kuhamisha mafuta zenye uwezo wa kusukuma lita 800,000 kwa saa ili kuongeza kasi ya kuhamisha mafuta kwenda kwenye maghala ya Kampuni za Mafuta (OMCs).

# 8

## Kuimarisha utendaji wa taasisi za Wizara, hasa TANESCO, EWURA na PBPA, na huduma zinazotelewa na taasisi hizo.

1. Serikali ilibadili madeni ya TANESCO yanayofikia Shilingi trilioni 2.4 kuwa mtaji wa Shirika hilo. Hatua hiyo itavutia uwekezaji pamoja na kuimarisha utendaji na mapato ya Shirika hilo.

2. TANESCO ilichukua hatua mbalimbali za kuimarisha utoaji wa huduma, ikiwemo kuwepo kwa kituo cha miito ya simu *(unified call centre)* ambacho kinafanya kazi saa 24; kuendelea kutumia mfumo wa maombi ya umeme wa Nikonekt ambao unawezesha wateja kuomba kuunganishiwa umeme hadi kufungiwa pasipo kufika ofisi za TANESCO; na kuanzishwa kwa mfumo wa Huduma ya Nihudumie ambao unatumika kuboresha huduma kwa wateja na kuwezesha utoaji wa taarifa kwa mteja kuhusu kushughulikiwa kwa suala alilowasilisha TANESCO hadi linapokamilika.

3. EWURA iliboresha mfumo wa *National Petroleum and Gas Information System* (NPGIS) unaowezesha Serikali kupitia Mamlaka hiyo kupata taarifa za hali ya upatikanaji wa mafuta nchini.

4. EWURA iliboresha mfumo wa kupokea maombi ya leseni za umeme, mafuta na vibali vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta *(Licensing and Order Information System – LOIS)*.

5. Serikali imeunda Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA inayoongozwa na Prof. Mark Mwandosya (Waziri Mstaafu) pamoja na kuteua Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hiyo.

6. EWURA imehuisha Kanuni mbili (2) za udhibiti, ambazo ni Kanuni ya Umeme ya Huduma za Ufungaji Mifumo ya Umeme – *The Electricity (Installation Services)* (*Amendment*) *Rules*, 2023 na Kanuni za Usimamizi wa Miundombinu na Biashara ya Mafuta - *The Petroleum (Wholesale, Storage, Retail and Consumer Installation Operations) (Amendment) Rules,* 2023. Lengo la uhuishaji huo ni kuongeza ufanisi katika utoaji wa leseni na kuwezesha wananchi kumudu gharama za huduma.

# 9

## Kuongeza ushiriki na uwekezaji wa Sekta Binafsi katika Sekta ya Nishati.

1. Serikali kupitia TANESCO imesaini Hati za Makubaliano (*Memorandum of Understanding – MoUs*) na Kampuni binafsi mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati jadidifu, gesi asilia na makaa ya mawe. Wawekezaji hao binafsi ni pamoja na: Total Eren (MW 200); Abu Dhabi FutureEnergy Company PJSC - Masdar (MW 2,000); Sumitomo (MW 300 – 600); Mbeya Power Ltd (MW 300) na Kilwa Energy (MW 318). Kazi za Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) zinaendelea kwa sasa ili Wawekezaji hao washiriki katika uzalishaji wa umeme.

2. Serikali imeanza taratibu za kuingia makubaliano na kampuni ya AFRICA50 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kwa mfumo wa wasafirishaji binafsi wa umeme *(Independent Power Transmission – IPT)*. Miradi hiyo ni Rufiji – Kibiti – Likong'o; Likong'o – Somanga Fungu; Mtwara – Tunduru – Songea; Segera – Same – Kisongo; na Kinyerezi – Somanga Fungu.

3. Serikali imeanza taratibu za kuingia makubaliano na wawekezaji binafsi ambao ni Larsen & Toubro Ltd na Gridworks Development Partners LLP kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Chalinze – Dodoma, Chalinze – Segera na Segera – Tanga pamoja na vituo vya kupoza umeme vyenye uwezo wa MVA 300 Segera, upanuzi wa kituo cha MVA 750 Dodoma *(bay extension)* na MVA 150 Tanga.

4. Serikali imeidhinisha bei elekezi za Kampuni sita (6) za wazalishaji wadogo wa umeme ambazo zinahamasisha na kuchochea uwekezaji wa Sekta Binafsi katika uzalishaji umeme. Kampuni hizo ni, Husk Power Limited, Watu na Umeme Tanzania Limited, POWERGEN Renewable Energy Limited, Jumeme Rural Power Supply, na POWERCORNER Tanzania Limited.

5. Wamepatikana waendelezaji watatu (3) wa miradi ya kusambaza umeme kwa kutumia nguvu ya jua katika visiwa 28 vilivyopo katika mikoa ya Kagera (8), Mwanza (13), Mara (3) na Lindi (4) na kuunganisha umeme kwa wateja 9,515

6. Serikali kupitia Wizara ya Nishati imesaini MoU na Kampuni ya ENOC LLC ya Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kwa ajili ya ujenzi wa kituo kikubwa cha kupokea na kuhifadhi mafuta jijini Dar es Salaam

# 10

## Kuhakikisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia unaimarika.

1. Jumla ya Watanzania 1,969 waliajiriwa kupitia ajira za moja kwa moja na Watanzania 160 waliajiriwa kwa ajili ya uchukuaji data za mitetemo za mfumo wa 3D katika Kitalu cha Ruvuma. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023, jumla ya Dola za Marekani milioni 134.6 sawa na Shilingi bilioni 313.14 zilitumika katika ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka soko la ndani.

2. Kampuni za ndani ziliendelea kutambuliwa na kusajiliwa katika Kanzidata ya *Local Suppliers and Service Providers* (LSSP) kwa ajili ya kupatiwa kipaumbele katika fursa zilizopo kwenye miradi mbalimbali hususan Mradi wa EACOP. Jumla ya Kampuni 1,748 zimesajiliwa katika kanzidata ambapo 190 zilipata fursa za kuuza bidhaa na kutoa huduma mbalimbali kwenye Mradi.

3. Kampuni ya kitanzania *(Solution Tag)* ilishinda zabuni ya kukagua na kusafisha bomba la gesi asilia (*intelligent pigging*) lenye urefu wa mita 800 linalotoa gesi asilia kutoka katika kisima hadi ulipo mtambo wa kuchakata gesi asilia wa Mnazi Bay. Kazi hii itahusisha vilevile kukagua na kusafisha bomba la kilomita 27 linalosafirisha gesi kutoka ulipo mtambo wa kuchakata gesi wa Mnazi Bay hadi kituo cha kupokea gesi asilia Mtwara mjini. Zabuni hii ina thamani ya takriban Dola za Marekani 500,000 sawa na Shilingi bilioni 1.6.

# 11

## Kufufua Shughuli za utafiti na utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

1. Shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia zimeendelea katika vitalu vya Mnazi Bay Kaskazini, Eyasi–Wembere, Songo Songo Magharibi, Ziwa Tanganyika na Vitalu Namba 4/1B na 4/1C.
2. Serikali inaendelea kudurusu Mkataba Kifani wa Uzalishaji na Ugawanaji wa Mapato (*Model Production Sharing Agreement* - MPSA) wa mwaka 2013 ili kuwa na MPSA mpya inayoendana na mazingira ya sasa na itakayovutia uwezekezaji wa Sekta Binafsi katika utafiti na uendelezaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia.
3. Serikali kupitia PURA inaendelea kuweka mipaka ya Vitalu vitakavyonadiwa na kuandaa Vifurushi vya Data *(Data Packages)* kwa kila Kitalu. Aidha, jumla ya Vitalu 26 vinafanyiwa uchambuzi ili kupendekezwa kuingizwa katika mnada, ambapo 15 vipo nchi kavu na 11 baharini.
4. Serikali kupitia PURA inatarajia kuendesha Duru ya Tano (5) ya kunadi vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia kati ya mwezi Desemba, 2023 hadi Machi, 2024 baada ya kukamilika kwa shughuli za maandalizi zinazoendelea.
5. Serikali kupitia PURA imekamilisha uandaaji wa rasimu ya Ramani ya Kidijitali (*Interactive Digital Petroleum Reference Map*) kwenye Mfumo wa Taarifa wa Kijiografia (*Geographical Information System – GIS*) inayotoa taarifa za Vitalu vya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini.

# 12


## Kuongeza matumizi ya nishati ya gesi kwa kupikia (LPG) na kwenye magari na viwandani (CNG).

1. Kumefanyika mjadala wa kitaifa wa Nishati safi ya kupikia tarehe 1 na 2 Novemba, 2022 na kwa sasa inakamilishwa Dira na Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia utakaozinduliwa mwezi Julai, 2023 na kuanza kutekelezwa
2. Serikali imetoa katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa Taasisi za umma na Binafsi zinazolisha zaidi ya watu 100 kuanzia mwezi Januari, 2024 ili kuimarisha matumizi ya nishati ambayo ni rafiki wa mazingira, ikiwemo gesi.




3. Jumla ya leseni mbili (2) za kampuni za gesi ya LPG na leseni 19 za mawakala wa Gesi ya LPG zilitolewa.
4. Vimetolewa vibali vitatu (3) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kujaza gesi asilia (CNG) katika magari yanayotumia nishati hiyo kwa Kampuni ya Taqa Dalbit Jijini Dar es Salaam, TP Company Ltd Bagamoyo na Dangote Cement Limited Mkuranga mkoani Pwani.
5. Vimetolewa vibali vitatu (3) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwa TPDC Jijini Dar es Salaam na Mnazi Mmoja Mkoani Lindi pamoja na Kampuni ya PanAfrican Energy Jijini Dar es Salaam.
6. Serikali kupitia REA imekamilisha taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi atakayebainisha aina ya nishati safi itakayotumika katika maeneo ya Taasisi za Umma.
7. Taratibu za ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika mikoa ya Lindi na Pwani itakayounganisha wateja 980 wa awali zinaendelea.
8. REA ilitangaza fursa za usambazaji wa mitungi ya gesi kwa sekta binafsi.
9. REA inakamilisha Mwongozo wa Usambazaji wa Majiko Banifu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia ambapo majiko 70,000 yatasambazwa katika maeneo ya vijiji na vijiji miji.
10. Ujenzi wa bomba la kusambaza gesi asilia lenye urefu wa kilomita 12.4 kutoka Mwenge hadi Mbezi Beach kupitia barabara ya Bagamoyo umefikia asilimia 44.2 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2023.
11. Ujenzi wa bomba la kusambaza gesi katika maeneo ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) na Mlimani City umeendelea ambapo migahawa mitatu (3) na maabara moja (1) katika chuo cha DUCE pamoja na migahawa kumi na mbili (12) iliyopo Mlimani City Mall itaunganishwa gesi.

## Ukuaji wa mahitaji ya umeme umeongezeka kutoka MW 832.55 mwaka 2010 hadi MW 1,431.59 Mwezi Mei, 2023



## Ujenzi wa Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Julius Nyerere (JNHPP), MW 2,115 umefikia asilimia 86.89, ikilinganishwa na asilimia 60.22 za mwezi Aprili, 2022





## Njia za Kusambaza Umeme Zimeendelea kuongezeka

| NA. | NJIA ZA USAMBAZAJI WA UMEME | UREFU (KM) | | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| | | MEI, 2022 | MEI, 2023 | |
| 1. | Njia za msongo wa kV 33 | 48,965.73 | 55,045.55 | 12.4 |
| 2. | Njia za msongo wa kV 11 | 12,648.73 | 12,986.25 | 2.7 |
| 3. | Njia za msongo wa kV 0.4 | 92,374.03 | 100,516.56 | 8.8 |
| **JUMLA** | | **153,988.49** | **168,548.49** | **9.5** |

## Maboresho ya Huduma kwa Wateja pamoja na mambo mengine, yamewezesha kuunganisha umeme kwa jumla ya wateja 4,319,258 hadi Aprili, 2023 ambapo mwezi Juni, 2022 kulikuwa na wateja 3,842,096 waliounganishiwa huduma hiyo









Mtambo wa kuchoronga visima vya uhakiki (drilling rig) kwa miradi ya jotoardhi umenunuliwa na kuwasili nchini



## 2.0 VIPAUMBELE VYA BAJETI YA MWAKA 2023/24

| NA. | KIPAUMBELE KATIKA |
|---|---|
| 1. | Kupeleka umeme katika vitongoji 36,101 vilivyosalia, sawa na asilimia 56 ya vitongoji 64,760 vya Tanzania Bara. |
| 2. | Kukamilisha miradi ya uzalishaji wa umeme ikiwa ni pamoja na Miradi ya Umeme wa Maji ya Julius Nyerere (MW 2,115) na Rusumo (MW 26.67) pamoja na kutumia gesi wa Kinyerezi I Extension (MW 185). |
| 3. | Kuendelea kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya umeme unaotokana na maji ikiwemo Ruhudji (MW 358), Rumakali (MW 222), Kakono (MW 80), Malagarasi (MW 49.5); Kikonge (MW 300); umeme unaotakana na gesi wa Mtwara (MW 300), Mradi wa Mawe (MW 150) na Mradi wa Mwamba (MW 450) na miradi ya nishati jadidifu ya jotoardhi, upepo na jua. |
| 4. | Kukamilisha miradi mbalimbali ya usafirishaji wa umeme ambayo utekelezaji wake unaendelea. |
| 5. | Kuhakikisha umeme wa uhakika unaendelea kupatikana nchini kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa *(National Grid Stabilization Project)* pamoja na kufikisha gridi ya Taifa katika Mikoa ya Kagera na Katavi. |
| 6. | Kukamilisha Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu *(REA III, Round II)* ambapo umeongezwa wigo wa njia za Msongo Mdogo kutoka kilomita moja (1) hadi kilomita tatu (3) na wateja kutoka 22 hadi 66 kwa kila kijiji; pamoja na Miradi ya Ujazilizi Awamu ya IIA (Densification IIA) na Peri Urban II. |
| 7. | Kutekeleza mradi wa Ujazilizi Awamu ya IIB na IIC (*Densification IIB* na *IIC*); Peri Urban III; kusambaza umeme katika migodi midogo, maeneo ya kilimo na viwanda pamoja na kusambaza umeme katika maeneo yaliyo mbali na gridi *(off – grid projects)*. |
| 8. | Kuanza maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG)*, ikiwa ni pamoja na kufanya stadi za awali za utekelezaji wa mradi (*Pre-Front End Engineering Design – Pre-FEED)* na masuala ya kihandisi na kisanifu *(FEED)*. |
| 9. | Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima - Uganda Hadi Tanga – Tanzania (EACOP); shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya Kimkakati; usambazaji wa gesi asilia viwandani, majumbani na nchi jirani; kuimarisha matumizi ya CNG katika magari pamoja na kunadi vitalu (*licencing round*) vilivyo wazi katika maeneo ya nchi kavu na baharini ili viendelezwe. |
| 10. | Kuendelea kutekeleza mikakati na programu mbalimbali za kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia *(clean cooking)* nchini pamoja uanzishwaji wa vituo vidogo vya mafuta vijijini. |
| 11. | Kuhakikisha nchi inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli pamoja na ufanisi katika kushughulikia bidhaa hizo kwa kutekeleza mikakati mbalimbali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kwa manufaa ya walaji na uchumi kwa ujumla. |
| 12. | Kuendelea kuimarisha Taasisi/Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya TANESCO, TPDC, EWURA na PURA pamoja na Taasisi Tanzu ili yatoe huduma bora kwa mujibu wa matarajio ya wadau, kuimarisha mapato pamoja na tija na ufanisi katika uendeshaji. |
| 13. | Kuimarisha ushiriki wa wadau husasan Sekta Binafsi katika uzalishaji na usafirishaji wa umeme, ikiwemo Kampuni za Africa 50, Gridworks na Larsen & Turbo na katika uendelezaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia. |
| 14. | Kuendelea kuimarisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia pamoja na rasilimali watu ya Wizara ya Taasisi zake na upatikanaji wa vitendea kazi muhimu. |

## 3.0 MIRADI YA KUZALISHA UMEME ITAKAYOTEKELEZWA MWAKA 2023/24

| NA. | MRADI UTAKAOTEKELEZWA | FEDHA ILIYOTENGWA (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115. | Trilion1.5 |
| 2. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Maji wa Ruhudji - MW 358. | Bilion 6.27 |
| 3. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Maji wa Rumakali - MW 222. | Bilioni 5.2 |
| 4. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Maji wa Kikonge - MW 330. | Milioni 500 |
| 5. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Maji wa Malagarasi - MW 49.5. | Bilioni 15.52 |
| 6. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Maji wa Kakono - MW 87.8. | Bilioni 36.53 |
| 7. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Jua wa Shinyanga - MW 150. | Bilioni 27.63 |
| 8. | Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia Gesi Asilia wa Mawe - MW 150. | Bilioni 345 |
| 9. | Ukarabati wa Kituo cha Kufua Umeme cha Hale | Bilioni 6.4 |

## 4.0 MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUSAMBAZA UMEME ITAKAYOTEKELEZWA 2023/24

| NA. | MRADI UTAKAOTEKELEZWA | FEDHA ZILIZOTENGWA (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Njia Kuu ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Singida-Arusha-Namanga. | Bilioni 15.91 |
| 2. | Ujenzi wa Njia Kuu ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma (TAZA). | Bilion 56.32 |
| 3. | Ujenzi wa Njia Kuu ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Kigoma - Nyakanazi. | Bilion 34.00 |
| 4. | Ujenzi wa Kituo cha Kupooza Umeme Shinyanga | Bilioni 2.700 |
| 5. | Ujenzi wa Njia Kuu ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Geita - Nyakanazi. | Bilioni 11.72 |
| 6. | Ujenzi wa Njia Kuu ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Benaco - Kyaka | Bilioni 5.800 |
| 7. | Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi. | Bilioni 3.84 |
| 8. | Ujenzi wa Njia Kuu ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere hadi Kituo cha Kupoza Umeme Chalinze. | Bilioni 20.50 |
| 9. | Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Gridi ya Taifa (TANESCO Transmission Grid Rehabilitation & Upgrade Project –TTGRUP) | Bilioni 29.61 |

## 5.0 MIRADI YA KUSAFIRISHA UMEME ILIYOPO KATIKA HATUA ZA UTAYARISHAJI

| NA. | MRADI UTAKAOTEKELEZWA | FEDHA ILIYOTENGWA (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kV 400 Sumbawanga – Mpanda – Kigoma | Milioni 100 |
| 2. | Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma | Milioni 500 |
| 3. | Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Segera – Same hadi Lemugur (Arusha). | Bilioni 2.5 |
| 4. | Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme (Submarine Cable) Msongo wa kV 220 kutoka Tanzania Bara (Ununio) hadi Zanzibar. | Bilioni 2.35 |
| 5. | Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme Manyoni (Manyoni Substation – MVA 60) | Milioni 100 |
| 6. | Mradi wa Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Tanzania hadi Uganda (Masaka - Ibadakuli) | Milioni 250 |

## 6.0 MIRADI YA KUSAMBAZA UMEME VIJIJINI ITAKAYOTEKELEZWA MWAKA 2023/24

| NA. | MRADI UTAKAOTEKELEZWA | FEDHA ZILIZOTENGWA (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (REA III Round II). | Bilioni 9.9 |
| 2. | Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji – (*Hamlet Electrification Project – HEP*) | Bilioni 377.05 |
| 3. | Mradi wa Ujazilizi Awamu ya Pili B. | Bilioni 24.76 |
| 4. | Mradi wa Kuwezesha Ujenzi wa Vituo Vidogo vya Kusambaza bidhaa za Mafuta ya Petroli Vijijini. | Bilioni 10.00 |
| 5. | Mradi wa Ufungaji wa Mifumo ya Umeme Jua kwenye Makazi Yaliyo Visiwani. | Bilioni 3.52 |
| 6. | Programu ya Kuwezesha Waendelezaji wa Miradi Midogo ya Nishati Jadidifu Vijijini chini ya Utaratibu wa Kusaidia Uandaaji wa Miradi (PPSF) | Bilioni 4.70 |
| 7. | Mpango wa Uendelezaji Miradi ya Nishati Jadidifu Inayofua Umeme kwa Kutumia Nguvu ya Maji. | Bilioni 5.0 |

# 7.0 MIRADI YA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI ITAKAYOTEKELEZWA MWAKA 2023/24

| NA. | MRADI UTAKAOTEKELEZWA | FEDHA ILIYOTENGWA (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mnazi bay Kaskazini | Bilioni 24.86 |
| 2. | Eyasi - Wembere | |
| 3. | Songo Songo Magharibi | |
| 4. | Ziwa Tanganyika | |
| 5. | VitaluNa. 4/1B na 4/1C | |

# 8.0 MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA GESI ASILIA NA MAFUTA ITAKAYOTEKELEZWA MWAKA 2023/24

| NA. | MRADI UTAKAOTEKELEZWA | FEDHA ZILIZOTENGWA (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (*Liquefied Natural Gas – LNG*). | Bilioni 6 |
| 2. | Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Ntorya (Kitalu cha Ruvuma) hadi Madimba. | Bilioni 58.75 |
| 3. | Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. | Bilioni 12.6 |
| 4. | Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Lindi na Mtwara. | Bilioni 1.6 |
| 5. | Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania (East African Crude Oil Pipeline - EACOP) | Bilioni 70.2 |

# BAJETI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2023/24

Jumla ya Bajeti ni **Shilingi 3,048,632,519,000** ambapo:

A. **Shilingi 2,960,702,821,000** sawa na **asilimia 97.1** ya Bajeti yote ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mchanganuo wa:
   - Shilingi 2,609,156,128,000 ni fedha za ndani; na
   - Shilingi 351,546,693,000 ni fedha za nje.

B. **Shilingi 87,929,698,000** sawa na **asilimia 2.9** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa mchanganuo wa:
   - **Shilingi 71,637,112,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC); na
   - **Shilingi 16,292,586,000** kwa ajili ya Mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

The United Republic of Tanzania
Ministry of Energy
Government City Mtumba, Nishati Street
P.O. BOX 2494, 40488 Dodoma, Tanzania.
Email Address: ps@nishati.go.tz
Phone: +255-26-2322018

nishati.go.tz